



TAARIFA KWA UMMA
KUANZA KWA UTEKELEZAJI WA KANUNI ZILIZOFANYIWA MAREKEBISHO -
TAREHE 01/07/2026

Dar es Salaam, 30 Juni, 2026

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inapenda kuutaarifu umma na wadau wa sekta ya usafiri ardhini kuwa, kwa kuzingatia **Kifungu cha 45 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 na kifungu cha 46 cha Sheria ya Utoaji wa Leseni za Usafirishaji Sura ya 317**, Kanuni zifuatazo zimefanyiwa marekebisho:

1. Kanuni za Huduma za Usafiri wa Kukodi za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Marekebisho) Tangazo la Serikali Na. 1082 la Mwaka 2024 na Marekebisho yake kupitia Tangazo la Serikali Na. 6 la Mwaka 2026;
2. Kanuni za Utoaji wa Leseni Leseni za Usafirishaji kwa Magari ya Mizigo (Marekebisho) Tangazo la Serikali Na. 1083 la Mwaka 2024 na Marekebisho yake kupitia Tangazo la Serikali Na. 7 la Mwaka 2026; na
3. Kanuni za Utoaji wa Leseni za Usafirishaji kwa Magari ya Abiria (Marekebisho) Tangazo la Serikali Na. 1084 la Mwaka 2024 na Marekebisho yake kupitia Tangazo la Serikali Na. 8 la Mwaka 2026.

Kanuni hizi na marekebisho yake zinapatikana katika tovuti ya LATRA www.latra.go.tz

Marekebisho haya yanalenga kuboresha ufanisi na uendeshaji ikiwa ni pamoja na kuboresha **makundi ya leseni, vyeti na vibali**; marekebisho ya **muundo na viwango vya ada za leseni** ili kuendana na uhalisia; marekebisho ya makosa na **adhabu** ikiwemo: kutoa **onyo kwa maandishi kabla ya kuchukua hatua ya kutoza faini**; na **kupunguza kiwango cha faini ya makosa kutoka Shilingi 250,000 hadi Shilingi 150,000** kwa makosa mbalimbali.

Aidha, utekelezaji wa Kanuni hizi unalenga kuboresha usalama, kulinda mitaji na kuongeza ufanisi wa watoa huduma, na kulinda ubora wa huduma na maendeleo endelevu ya sekta ya usafiri ardhini nchini. Hivyo, LATRA inawahimiza wadau wote wanaohusika na umma kwa ujumla **kujielimisha kuhusu marekebisho haya na kuyazingatia kikamilifu.**

Pamoia kwa Usafiri Bora

Salum S. PAZZY

MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO - LATRA